

# ITILIMA DC



## KAMATI ZA TAALUMA MNAJUKUMU LA KUIFANYA ITILIMA ING'ARE KITAALUMA: AFISA ELIMU MKOA



Afisa Elimu Mkoa wa Simiyu Ndg. Hinju Kimweri akiongea na Wadau wwa Elimu Wilayani Itilima

Afisa Elimu Mkoa wa Simiyu (R.E.O) Ndg. Hinju Kimweri awataka wajumbe wa kamati za taaluma wilayani Itilima kuhakikisha Itilima inang'ara kitaaluma katika matokeo yajayo ya mitihani ya majaribio na Kitaifa.

Akiongea katika kikao kazi cha tathmini ya Elimu kilicho fanyika Wilayani Itilima na kuzinduliwa na Mkuu wa Wilaya ya Itilima Mhe. Benson Kilangi, Afisa Elimu Mkoa aliwataka wadau hao wa Elimu

Kuutekeleza Mkakati wa Taaluma wa Mkoa na wa Halmashauri kivitendo.

Mkakati huo wenye Vipengele 11, kikiwemo kipengele cha Makambi ya Taaluma, R.E.O alisema

“Makambi haya yaliyoasisiwa na Mkuu wetu wa Mkoa Mhe. Anthony Mtaka ni muhimu sana kwetu na umuhimu wake umeanza kujidhihirisha katika matokeo ya mitihani kwa mwaka 2018, kwa Mkoa wa Simiyu kushika nafasi ya 9 kati ya Mikoa 31,

huku Halmashauri ya Bariadi Mji ikishika nafasi ya 9 huku Halmashauri ya Itilima ikishika nafasi ya 11, kati ya Halmashauri 186 matokeo haya ni ishara ya kuwa kazi ilifanyika katika makambi hayo ya taaluma”

Aidha akizungumzia suala la motisha kwa Walimu na kwa wanafunzi waliyofanya vizuri R.E.O alisema

“kuwapa motisha wanaofanya vizuri kwanza ni moja ya utekelezaji wa Mkakati wa taaluma, pili kuwajenga walimu na

wanafunzi katika kujituma, tatu kuipandisha Wilaya, na kuunyanyua Mkoa na ndiyo maana Mkuu wetu wa Mkoa Mhe. Anthony Mtaka alitoa Motisha kwa wanafunzi na Walimu waliyofanya vizuri katika matokeo ya Kidato cha Nne Kimkoa siku ya Elimu pale Nkololo”

Akiongea kwa niaba ya Chama Cha Walimu Mkoa (CWT) Katibu wa CWT Mkoa Ndg. Said Mselem alisema “Walimu Mnapaswa Kutimiza wajibu wenu ili kazi ya kuwatetea

mnapoteleza iwe rahisi na mnapaswa kujiepusha na mikopo isiyo na tija, utoro kazi-ni, na kujiepusha na mahusiano ya kimapenzi na Wanafunzi wenu, endapo ikathibitika unajihusina katika mapenzi na mwanafunzi wako sisi hatuta kuwa na jinsi ya kutetea na utafungwa tunakuangalia”

Aidha Bw. Mselem alisema yakuwa wadau wa Elimu tunapaswa kuheshimiana kwani hakuna Afisa elimu kama hakuna Walimu, hautaitwa Mwalimu kama hakuna Wanafunzi na vile vile hakuna CWT kama hakuna Walimu sisi sote tunategemeana, hivyo basi tuna kila sababu ya kuheshimiana.

Tathmini hiyo ya masuala ya Kitaaluma ili husisha utoaji wa zawadi kwa shule zilizo fanya vizuri ki wilaya na ili-jumisha wadau mbalimbali wa Elimu kutoka ofisi ya Afisa Elimu Mkoa, Chama Cha Walimu Mkoa, Mthibiti Ubora wa Elimu wilaya ya Itilima, TSC- Itilima, Maafisa kutoka ofisi ya Mkurugenzi Itilima wakiongozwa na Maafisa elimu Sekondali na Msingi.



**Wadau wa elimu wakifuatilia tathimini ya maendeleo ya Elimu wilayani Itilima**



**Mkuu wa Shule ya Sekondari Shishani Ndg. Sollo Thomasmon akipokea Zawadi kwa niaba ya Shule yake kufanya vizuri katika matokeo ya kidato cha nne na kuongoza kiwilaya**



**Mkuu wa Wilaya ya Itilima Mhe. Benson Kilangi akibadilishana mawazo na Viongozi wa Elimu Mkoa wa kwanza kushoto Afisa Taaluma Mkoa Ndg. Onesmo Simime akifuatiwa na afisa Elimu Mkoa Reo ndg. Hinju Kimweri,, wakwanza kulia kulia Katibu Mkoa CWT, akifuatiwa na afisa Elimu Wilaya Itilima Edward Mtobi**